Mhariri anakaribisha barua na makala fupi kutoka kwako msomaji kuhusu masuala ya babrabara na usafirishaji. Barua ziwe fupi na zinazoeleza suala moja kwa moja na zitumwe kwa Mhariri, Tanzania Roads S. L. P 12497 Dar es Salaam, au kwa barua pepe kwa roadfund@raha.com au ckidanka@regaliamedia.com. Tutachapisha barua zinazofikia kiwango tunachokitaka na zilizo na jina na anuani ya mwandishi. Ikiwa hupendi jina lako litokee kwenye jarida, tueleze hivyo. Unakaribishwa pia kuleta kichekesho kwa ajili ya safu hii.

Vigezo vya ufanisi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara

Inaendelea kutoka Uk 9



Utunzaji rasilimali ukipimwa kwa mahitaji yote ya ukarabati yakilinganishwa na bajeti



Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ufupi

WAJIBU WA BODI YA MFUKO WA BARABARA

kuhakikisha makusanyo kamiliifu ya mapato ya mfuko

kugawa fedha kwa wakala wa utekelezaji

kusimamia matumizi ya fedha kuhakikisha thamani yake katika kazi

VYANZO VYA MAPATO

Tozo ya mafuta inachangia asilimia 96

Malipo ya mizigo ya nje


Faini za kuzidisha uzito

Vigezo vya ufanisi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara


Ufanisi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara hupimwa kwa kutumia vigezo vilivyoandaliwa chini ya mradi uliobuniwa na kufadhiliwa na Bank ya Dunia unaoitwa “Sub-Saharan Africa –Transport Policy Programme” ambao ulibuni mpango wa matengezo ya barabara kwa nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara. Aidha ufanisi wa Mfuko unapimwa pia na malengo ya MKUKUTA kama yalivyoainishwa kwenye kitabu cha MKUKUTA II.

Malengo ya vigezo hivyo ni kuongoza kutathmini ufanisi wa Mfuko kwa kuangalia (i) **kiwango cha maboresho** kinachopimwa kwa mchango tozo kwa watumiaji wa barabara na mchango wa tozo za mafuta kwa Mfuko wa Barabara, (ii) **utunzaji wa barabara kama rasilmali** unaopimwa kwa kiwango cha mahitaji ya ukarabati wa kawaida, kiwango cha mahitaji yote ya ukarabati; ukilinganisha na bajeti inayotengwa (iii) **Nia ya dhati ya Serikali katika Maboresho** inayopimwa kwa kiwango cha fedha zinazotengwa kila mwaka kikilinganishwa na bajeti; (iv) **Ufanisi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara** unaopimwa kwa utoaji wa fedha kwa wakati kwa wakala wa utekelezaji.




Ulinganifu kati ya tozo zinazolipwa na watumiaji wa barabara na tozo za mafuta




Kiwango cha Maboresho kikipimwa kwa mchango wa Tozo za Mafuta kikilinganishwa na Mapato yote ya Mfuko



Utunzaji wa rasilimali ukipimwa na Mahitaji ya Ukarabati wa Barabara ukilinganishwa na Bajeti



Utunzaji wa rasilimali ukipimwa na Mahitaji ya Ukarabati wa Barabara ukilinganishwa na Bajeti



RFB kutoa bilioni 127/- TAMISEMI

Bodi ya Mfuko wa Barabara imetenga kiasi cha Tsh. 127,610,208,637.20 katika mwaka wa fedha 2012/13 kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa madhumuni ya ujenzi wa barabara zinazosimamiwa na serikali za mitaa nchi nzima.

Mkataba wa Kiutendaji kati ya Bodi na TAMISEMI kuhusu matengenezo ya barabara za wilaya, miji na za ujazio pamoja na ujenzi wa barabara mpya uliosainiwa kati ya taasisi hizo mbili unaeleza kuwa Bodi itatoa fedha hizo kwa ajili ya matengenezo na ujenzi wa barabara mpya ikiwa ni pamoja na kugharamia shughuli za utawala zinazohusiana na kazi hizo na usimamizi wake.

“Bodi itakuwa na majukumu ya kutoa kwa TAMISEMI kiasi cha fedha kili-chokubaliwa na kinachohitajika kwa wakati na kulingana na Mpango wa Fedha wa TAMISEMI 2012/13, na kulingana na taratibu za utoaji fedha za Bodi,” inasomeka sehemu ya Makubaliano hayo na kuongeza kuwa fedha za barabara zitakazotolewa chini ya makubaliano hayo lazima zitumike kwa malipo ya kazi zilozifanyika katika mwaka wa fedha 2012/13 kwa mujibu wa mpango-kazi.

Utoaji fedha utakuwa kama ifuatavyo: Tshs. 102,541,450,000 kwa kazi za ukarabati wa barabara; Tshs. 4,474,760,000 kwa matumizi ya dharura; Tshs. 1,704,000,000 kwa shughuli za Makao Makuu ya TAMISEMI; Tshs. 12,761,002,000 kwa miradi ya maendeleo ya barabara; Tshs. 4,852,000,000 kwa gharama za usimamizi wa Halmashauri; na Tshs. 1,276,100,000 kwa ufuatiliaji na utawala. Jumla: Tshs. 127,609,321,000.

Makubaliano hayo yanasisitiza kuwa TAMISEMI na Halmashauri zitawajibika kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa zinatumika kwa kufuata bajeti ya mpango-kazi kwa mujibu wa vigezo vya utendaji katika utekelezaji wa makubaliano hayo.

“TAMISEMI inaweza kubadili matumizi ya fedha kwenye bajeti kwa kiasi cha asilimia 10 kwa kipengele na matumizi yasiyidhi bajeti ya jumla. Ikiwa

itaonekana kuwa matumizi ya kipengele cha bajeti yanazidi asilimia 10 au zaidi, au kazi mpya ambazo hazikuwekwa kwenye mpango-kazi zinapaswa kutekelezwa, au kutokana na vikwazo vingine vya kifedha au kiutendaji kunajitokeza tatizo, TAMISEMI inaweza kuamua kubadili matumizi ya fedha hizo baada ya kushauriana na kukubaliana na Bodi.”

Inapotokea fedha zilizotolewa kwa mujibu wa makubaliano haya zinabaki, makubaliano yanataka aliyepokea fedha kutoa taarifa kwa Bodi na kuomba idhini ya kutumia fedha hizo kwa matumizi mengine.

Makubaliano hayo yanaelekeza kuwa TAMISEMI inapaswa kufanya juhudi za makusudi kutumia fedha zote katika mwaka husika wa fedha, na hivyo kupunguza kadiri iwezekanavyo kuwepo kwa fedha zinazolinga mwaka mwingine

wa fedha. “Fedha zinazobaki zinapaswa kutumika katika mwaka mpya wa fedha kumalizia mradi uliotengewa fedha hizo. TAMISEMI inapaswa kupata idhini ya Bodi kutumia fedha zilizobaki kwa matengenezo ya dharura ya barabara ndani ya mwezi mmoja tangu kuanza kwa mwaka mpya wa fedha.”

Katika makubaliano hayo, TAMISEMI inatakiwa kufanya juhudi kubwa kuhakikisha kuwa fedha zinatumika katika mwaka husika wa fedha, na matatizo mengine ya nje ya TAMISEMI kama vile ukosefu wa wakandarasi na vifaa yanashughulikiwa. Inatazamiwa kuwa kwa kufanya hivyo, fedha zinazobaki hazitakuwa zaidi ya asilimia 25. Fedha zote zilizowekwa kwa ajili ya ujenzi zita-tolewa kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa Juni 30, 2012. ■



Naibu Meneja, Utafutaji Rasilimali wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Eliud Nyahenga akiwasilisha mkataba wa huduma kwa wateja katika Mkutano wa Wadau wa barabara hivi karibuni

RFB kutumia nyenzo mpya kupima thamani ya fedha

Inatoka uk. 6

alieleza kwamba upimaji wa tathmini ya thamani ya fedha inatolewa kwa njia ya maoni, tofauti na nyenzo ya zamani ambapo asilimia ilitumika. Maoni kwa ajili ya mradi mmoja mmoja ni kwamba Nzuri ni kwa alama 2.6 – 3.0; Kutosheleza ni kwa alama 1.7 – 2.5; na Kutotosheleza ni kwa alama chini ya 1.7.

Thathmini ya thamani ya fedha kwa mradi mmoja mmoja inayotekelezwa na

taasisi ya barabara inaweza kutumika kupima utendaji wa taasisi husika. Ili kupima utendaji wa taasisi, alama za tathmini ya thamani ya fedha hupatikana kwa kuzingatia alama za mradi mmoja mmoja pamoja na gharama husika ya miradi.

Nyenzo mpya ilianza kutumika katika mwaka wa fedha 2011/2012 katika ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya kazi za barabara zilzofanyika mwaka

2010/2011 na 2011/2012.

Hata hivyo nyenzo mpya imekuwa na mapungufu ikiwemo kuhitajika mkaguzi kufanya uamuzi wa alama ya kuweka kwa kuzingatia busara yake. Kwa kazi za matengenezo ya kawaida, baadhi ya vigezo kwenye nyenzo hazihitajiki. Nyenzo hii inatumika kwa ajili ya kukagua miradi tu na kuwa haichunguzi kama mifumo ya kitaasisi iliyopo inafaa kuwezesha kuwepo kwa thamani ya fedha

kwa kuangalia viwango vya wafanyakazi, majukumu ya wafanyakazi, uratibu na kanuni za kiutawala inahakikisha kuwepo na kuboreshwa kwa thathmini ya thamani ya fedha.

Mhandisi Lwakatare alieleza kuwa nyenzo hiyo itakuwa inarekebishwa kila baada ya miaka miwili ili kuiboresha na utatarishwa mwongozo wa kuitumia. ■

Halmashauri lawamani kwa fedha za barabara

Wakaguzi wa hesabu wamegundua kuwa kiasi cha Sh 100,547,857 zimehamishwa kutoka akaunti ya Mfuko wa Barabara kwenda akaunti zingine

Sehemu ya taarifa ya Mkaguzi Mkuu na Mdhhibiti wa Serikali iliyotolewa na Bodi ya Mfuko wa Barabara kuhusu Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2010; inaonesha kiwango kikubwa cha matumizi mabaya na uhamishaji wa mamilioni ya shilingi.

Taarifa hiyo ilitolewa kama mada katika mkutano wa TAMISEMI na wadau wa barabara ulioofanyika jijini Arusha hivi karibuni.

Ukaguzi wa hesabu uliofanywa kwenye nyaraka za kumbukumbu za fedha za Halmashauri zilizopokea fed-

ha za Mfuko, umegundua kuwa Sh 31,043,184 zilitumika kwa matumizi ambayo hayahusiani na shughuli za barabara. Hii inaashiria kwamba miongozo ya Bodi ya Mfuko wa Barabara inakiukwa.

Kadhalika, ukaguzi huo umegundua kuwa kiasi cha Sh 476,066,839 zimetumika nje ya utaratibu wa kuandikiwa vocha ambapo nyaraka za malipo ya kiasi hicho cha fedha hazikutolewa kwa ajili ya ukaguzi kinyume cha Kifungu 45 (5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982.

“Kutokuwepo kwa vocha za malipo, mazingira ya mali-

po na matumizi ya fedha za kwenye akaunti hakukuthibitisha kuwa matumizi hayo ya Mfuko wa Barabara yalikuwa sahihi. inasema sehemu ya taarifa hiyo ambayo ‘Tanzania Roads’ inayo.

Katika kile kinachoonkana kuwa ni udhaifu wa usimamizi na udhibiti wa bidhaa na manunuzi, wakaguzi hawakukuta taarifa zozote zinazothibitisha kuwa bidhaa zilizonunuliwa zilitumika kwa maslahi ya umma. Maafisa wa bohari waliagiza bidhaa na kulipa Sh 60,805,852 ambazo hazikuonekana kwenye nyaraka na kumbukumbu za fedha

na matumizi yake hayakujulikana.

“Kwa mujibu wa taarifa hiyo, fedha zinazosemeka kutumiwa vibaya ni pamoja na Sh 1,033,544,112 zilizotolewa bila vocha; malipo zaidi kwa wakandarasi Sh 30,374,527; ucheleweshaji wa kumaliza kazi kwa wakandarasi Sh 3,505,775,545 na malipo yaliyotolewa stakabadhi zisizo rasmi Sh 132,539,250.

Wakaguzi pia waligundua kuwa kiasi cha Sh 100,547,857 zilihamishwa kutoka akaunti ya Mfuko wa Barabara kwenda akaunti zingine, ama kwa makosa au kwa kukopwa. Hadi wakati wa ukaguzi wa hesabu hizo, fedha hizo zilikuwa bado hazijarejeshwa kwenye akaunti ya mfuko wa barabara.

Taarifa hiyo ya ukaguzi wa hesabu pia inasema kuwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya zililipa kiasi cha Sh 117,907,980 kwa wakandarasi kwa kazi ya ukarabati, wakati Mikataba ya malipo hayo haikupatikana kwa ajili ya ukaguzi, kama ilivyotakiwa na Sheria. Kwa hiyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa kutokana na kutokuwepo kwa nyaraka hizo, inasomeka sehemu ya taarifa.

Taarifa hiyo inahitimisha: “Taarifa ya ukaguzi wa kina iliyowasilishwa ilifikishwa pia kwenye mengineji za Halmashauri husika katika vikao vya baada ya kumaliza ukaguzi ambapo masuala hayo yalijadiliwa na kufikiwa makubaliano kuwa ndivyo yalivyokuwa. Mengineji za Serikali za Mitaa ziliahidhi kuchukua hatua stahiki na kurekebisha makosa hayo. ■



Ofisa wa TAMISEMI anayeshughulikia barabara, Mhandisi Elina Kayanda akiwasilisha mada kuhusu utendaji wa Halmashauri katika miradi ya matengenezo ya barabara

Bodi ya Mfuko wa barabara kutumia nyenzo mpya

Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) imeanza kutumia nyenzo mpya ya kutathmini thamani ya fedha (VfM) ili kukagua jinsi fedha zinazotolewa na Bodi hiyo zinavyotumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Nyenzo hiyo iliyoboreshwa ni matokeo ya mkutano wa wadau uliofanyika Aprili 2011 ambao ulijadili nyenzo iliyokuwepo ambayo ilitumika kwenye ukaguzi wa kiufundi kwa kazi zilizofanyika mwaka wa fedha 2009-2010, ambayo

ilionekana kuwa na udhaifu na hivyo kutakiwa kuboreshwa. Nyenzo mpya, ilianza kutumika Julai mwaka 2011.

Akitoa mada katika mkutano wa wadau wa barabara jijini Arusha tarehe 31 Julai mwaka 2012, Mhandisi Ronald Lwakatare alibainisha kuwa nyenzo mpya ya VfM imebaki na baadhi ya miundo iliyokuwa ikitumiika katika nyenzo ya awali ikiwemo muundo wake wa jumla. Nyenzo mpya ina viashiria vitano zinazotumika kutathmini thamani ya fedha

katika hatua mbali mbali ya utekelezaji wa mradi zikiwa ni Mipango, usanifu na kuandaa nyaraka za manunuzi; taratibu za Manunuzi; Usimamizi wa mradi; Kukamilika kwa mradi; na Utekelezaji na ubora wa kazi. Kila kiashiria ina vigezo vinavyozingatia matokeo muhimu ya kutathmini thamani ya fedha inayotokana na kuiga uzoefu bora kutoka sehemu mbali mbali duniani.

Utekelezaji na ubora wa kazi umepewa uzito mkubwa kuliko viashiria

vyote kwa kuwa na asilimia 40, ikifuatiwa na Mipango, usanifu na kuandaa nyaraka za manunuzi asilimia 20%; Usimamizi wa mradi asilimia 20; taratibu za Manunuzi asilimia 10; na Kukamilika kwa mradi asilimia 10. Vigezo hufanyiwa uhakiki katika skeli ya namba moja hadi tatu, tatu ikimaanisha utendaji mzuri, mbili utendaji wa wastani, na moja utendaji mbovu.

Mhandisi Lwakatare

Inaendelea uk 7

RFB yajizatiti kutoa huduma bora zaidi

Bodi ya Mfuko wa Barabara imewahakikishia wateja wake kuwa imejizatiti kutoa huduma zake kwa weledi, uaminifu na uwajibikaji.

Hakikisho hilo lililotolewa katika mkutano wa wadau wa barabara uliofanyika jijini Arusha Agosti mwaka huu, na limeainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja ulio-wasilishwa na Bodi hiyo. Mkataba huo uliojadiliwa na wadau na kukubaliwa unaeleza wajiibu wa Bodi katika masuala yanayohusu mawasiliano, utoaji wa fedha na ufuatiliaji kwa wadau mbalimbali kama vile Wizara ya Ujenzi, Wakala wa Barabara –Tanzania (TANROADS) na Serikali za Mitaa.

Bodi imeahidi kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo na kutoa majibu ya haraka na sahihi kwa maswali ya wateja huku ikizingatia maadili, kukubali kuwajibika kwa vitendo vyake, na kujifunza kutokana na makosa yake.

“Bodi itajali wateja, na itashirikiana na wateja pamoja na wadau kutekeleza majukumu kama inavyotarajiwa na Serikali. Bodi itafanya majadiliano na wadau na wateja mbalimbali ili kupata maoni kuhusu mwelekeo wa kisera wa baadaye,” inasema sehemu ya Mkataba huo.

Vilevile, Bodi imeahidi kuwa itazingatia kuhakikisha kuwa thamani ya fedha zilizotolewa inaonekana katika miradi ya matengenezo na ukarabati wa

barabara inayotekelezwa.

Katika kuhakikisha utoaji wa taarifa unafanyika kwa haraka na umakini, Bodi imeahidi kujibu barua ndani ya siku tano za kazi, barua pepe zitajibiwa ndani ya siku tatu (isipokuwa zile zinazohitaji kufanyiwa utafiti zaidi na maamuzi kuchukuliwa na viongozi wa juu) na simu zitajibiwa mara moja.

Viwango vya Huduma kwa Wadau

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Bodi ya Mfuko wa Barabara inaahidi kutoa ushirikiano unaohitajika kwa ofisi hiyo katika mchakato wa ukaguzi wa hesabu; kama vile kuwasilisha taarifa za fedha ndani ya siku 90 baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha, na kuhakikisha kuwa sheria ya manunuzi ya umma inazingatiwa.

Kwa Wiraza ya Ujenzi, Bodi imeahidi kuwa Taarifa za Mwaka zitawasilishwa ndani ya siku 180 baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha, kumshauri Waziri anayehusika na barabara kuhusu vyanzo vipya vya tozo za barabara, kurekebisha viwango katika kanuni za ukusanyaji wa tozo za barabara na kuhudhuria mikutano ya mashauriano kwa mujibu wa ratiba.

Aidha Bodi imeahidi kutengeneza na kurekebisha mara kwa mara kanuni ya utengaji wa fedha miongoni mwa Wakala na kumshauri kwa usahihi Waziri anayehusika na barabara; ikiwa ni pamoja

na kutenga asilimia 10 ya fedha kwa ajili ya uendelezaji wa barabara.

TANROADS, TAMISEMI na Serikali za Mitaa zimehakikishiwa kuwa Bodi ya Mfuko wa Barabara itahakikisha fedha za kufanyia matengenezo ya barabara zinatolewa ndani ya siku tatu baada ya fedha hizo kuwa zimeingia katika akaunti ya benki ya Bodi, na makubaliano ya utendaji yataandaliwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha (kwa kawaida ni mwezi Juni) kwa ajili ya kuyapitia na kutoa maoni.

Bodi pia imeahidi kuhakikisha kuwa taarifa za matokeo ya Ukaguzi wa Kiufundi uliofanyika itatolewa kwa Wakala wa Utekelezaji ndani ya mwezi mmoja tangu kupokelewa kwa taarifa hizo na kufuatilia mara kwa mara utendaji wa TANROADS na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mkataba huo pia una vipengele vinavyoweke bayana majukumu ya wadau kama vile **Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**, Wizara ya Ujenzi, TAMISEMI, TANROADS na Halmashauri za Miji na Wilaya.

Kwa mujibu wa Mkataba huo, **Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali** anatarajiwa kukagua hesabu na kutoa taarifa za fedha kwa Bodi kwa wakati, na kushauri namna bora ya kuendesha Mfuko.

Wizara ya Ujenzi, inatarajiwa kuendelea kutoa msaada na maelekezo kwa Bodi na

kufanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Bodi kuhusiana na uendeshaji mzuri zaidi wa Mfuko.

TAMISEMI, itatarajiwa kusimamia majukumu ya Halmashauri ya ukarabati barabara, kuhakikisha uwepo wa wafanyakazi wenye sifa na uwezo, pamoja na kujenga uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutekeleza mapendekezo kutoka katika Bodi kuhusu masuala ya matumizi ya fedha katika halmashauri hizo.

TANROADS na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwa na taarifa kamili kuhusu kanuni za ukarabati barabara, kabla ya Mkataba wa Utendaji haujasainiwa kati yake na Bodi, ili kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi katika utendaji kazi.

Aidha TANROADS na Serikali za Mitaa zinatakiwa, pamoja na mambo mengine, kuhakikisha kuwa makadirio ya bajeti za matengenezo ya barabara zinawasilishwa kwenye Bodi kwa wakati bila kuchelewa. Wakati wa utekelezaji, watahakikisha kuwa thamani ya fedha inaonekana katika kupanga, kusanifu, kutumia kanuni za manunuzi, utekelezaji wa matakwa ya mikataba na uhibiti ubora wa gharama zisizo za lazima.

Wakandarasi wafungwa kwa kukiuka masharti

Jumla ya kampuni za ukandarasi 32 za ujenzi na watu binafsi wawili wamefungwa kufanya kazi ya ukandarasi kwa mwaka mmoja kutokana na makosa mbalimbali likiwemo la kulipwa kwa ‘kazi hewa’.

Orodha iliyotolewa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma na Ugavi (PPRA) wakati wa Mkutano wa TAMISEMI, Bodi ya Mfuko wa Barabara na Wadau wa barabara mjini Arusha hivi karibuni ilibainisha kuwa kampuni hizo pamoja na wakandarasi binafsi wamefungwa kuanzia Juni 22, 2012 hadi Juni 21, 2013.

Kampuni hizo pamoja na wakandarasi binafsi wanatoka mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Mtwara, Mbeya, Njombe na Dodoma.

Wakati wakandarasi binafsi, Zephania Ngeleja wa

Ukerewe na Grace Mbilinyi wa Njombe wamefungwa kwa kushindwa kufanya kazi ya kukusanya mapato katika kisikwa cha Malelema (Ngeleja) na kushindwa kutimiza masharti ya mkandarasi ya kukusanya mapato katika Lango la Idosi (Mbilinyi), kampuni nyingi zilizofungwa zimejipatia zaidi ya Sh milioni 200 kama malipo zaidi ya yaliyohitajika kwa kazi walizofanya ama malipo kwa ‘kazi hewa’.

Hata hivyo, zipo kampuni ambazo zina hadithi tofauti, nyingine zikiwa zimeteteleza kazi na kuondoka kabla ya kazi kumalizika kwa mujibu wa mkataba.

Muson Engineering Ltd ya Dodoma ilipewa kandarasi na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kwa ajili ya kujenga eneo la Mnadani lakini baadaye iligundulika kuwa viwango vilivyotumika katika ujenzi

huo vilikuwa duni kulingana na kiasi walicholipwa.

“Ukaguzi wa eneo la kazi uligundua kuwa kazi ilikuwa imekamili lakini michoro ya kazi hiyo ilitofautiana sana na kile ambacho kilifanyika eneo la kazi. “Mabadiliko hayo hayakuwa yamerekodiwa wala kukubalika na hivyo kufanya kuwa vigumu kwa Wakaguzi kulinganisha kiwango kilicholipwa, vipimo halisi katika michoro iliyo kwenye mkataba na vipimo halisi sehemu iliyojengwa. Kiwango cha malipo kilichoizidishwa kwenye malipo kinakadiriwa kuwa Sh. milioni 9,” inasomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Man – Ncheye Pa Co. Ltd ya Bunda imefungwa kwa kudaiwa kulipwa isivyo halali kiasi cha Sh. milioni 24.4 na Halmashauri ya Wilaya ya Magu “kwa kazi ambayo hawakuifanya kabisa”.

“Ingawa baadhi ya kazi za ujenzi wa mfumo wa majitaka na matengenezo ya barabara ya Ng’haya – Bugatu ilithibishwa na kumlipa mkandarasi, wakaguzi hawakuona ujenzi wowote eneo la kazi.

Kampuni nyingine ambazo zimetuhumiwa kulipwa fedha ambazo hawakustahili ni Jossam and Co. Ltd ya Karagwe, Satellite Contractors Co. Ltd ya Dodoma, Tenco Construction Ltd ya Morogoro na Icon Engineers ya Mwanza.

Wakati Jossam and Co. Ltd ililipwa malipo yasiyo halali ya Tsh 17.3 milioni na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa kazi ambayo haikufanyika, Satellite Contractors Co. Ltd ililipwa kiasi cha Tsh 94.6 milioni na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa kazi ambazo hazikufanyika. ■

Magufuli na rushwa Mizani

Inatoka uk 4

na watu ni gari moja watu kwa wanne.

Dkt. Magufuli alisema kuwa hivi sasa kuna magari yaliyosajiliwa yanakadiriwa kuwa 1,000,000 katika jiji la Dar es Salaam pekee, ambalo kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 lilikadiriwa kuwa na wakazi 4,000,000.

Huku magari yaliyopo tayari yakiendelea kusababisha msongamano; magari zaidi yamejazana bandarini yakisubiri kutolewa, huku mengine yakiwa njiani kuja nchini.

“Ndio maana tunapaswa kufanya kazi pamoja kuhakikisha kuwa tunapanua Jiji na kujenga barabara mpya ili kupunguza msongamano unaotokana na ongezeko la magari,” alisema Waziri.

Kwa mujibu wa Dkt. Magufuli, miradi mingi ya ujenzi wa barabara jijini Dar es Salaam na usumbufu uliopo haukupukiki kwa kuwa hifadhi za barabara jijini Dar es Salaam ni tofauti na zile za mikoani.

“Hapa Arusha na mikoa mingine hifadhi ya barabara ni mita 30 kutoka katikati ya barabara lakini Dar es Salaam ni mita 100 kwa pande zote kwa barabara kuu kama ile ya Morogoro,” alisema Dkt. Magufuli.

Waziri alibainisha kuwa ubomoaji wa nyumba za makazi na za biashara zilizo katika hifadhi ya barabara ni zoezi endelevu na wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa kufuata sheria.

“Ingawa magari zaidi na zaidi yanaendelea kuingizwa nchini, Serikali haina haja ya kuzuia uingizwaji huo. Chukulia mfano wa Dar es Salaam, magari milioni moja lazima yatahitaji madereva milioni moja kuyaendesha na hivyo kuongeza fursa za ajira,” alisema Dkt. Magufuli.

Alisema kuwa magari ya usafiri wa umma na ya binafsi yote yanaongeza fursa za ajira ikiwa ni pamoja na madereva, makondakta, mafundi gereji na wahudumu wa vituo vya mafuta.

Fungueni jiji la Arusha

Dk. Magufuli alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Magesa Mulongo na Meya wa Manispaa ya Arusha Gaudence Lyimo kuanza kufanyia kazi vituo vipya vitatu vya mabasi kwa ajili ya kuhudumia jiji la Arusha.

“Arusha imesongamana na mahali vilipo vituo vya sasa vya mabasi ambapo ni katikati kabisa ya mji, inachangia foleni isiyo ya lazima wakati mabasi yanayokwenda masafa marefu yanapolazimika kwanza kuingia mjini,” alisema Waziri na kuongeza kuwa wakati umefika kwa Arusha kuwa na vituo vipya vya mabasi.

“Kituo cha basi katikati ya mji kinapaswa kuhamishiwa mahali kama barabara ya Moshi Arusha na kihudumie mabasi yanayokwenda Moshi, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini,” alisema.

Dkt. Magufuli pia alishauri kituo kingine cha mabasi kijengwe barabara kuu iendayo Dodoma, kuelekea Kisongo ambapo mabasi kutoka Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa huleta abiria kuto-



Waziri wa Ujenzi, Mh John Magufuli akifungua Mkutano wa Wadau wa barabara jijini Arusha

ka Mwanza, Shinyanga, Singida, Babati na Dodoma.

Waziri pia aliwataka watendaji wa Jiji kujenga kituo kingine cha tatu kwa ajili ya mabasi ya masafa mafupi na daladala.

Jijini Arusha, mabasi ya abiria yasiyopungua 100 huingia kila siku na kufanya kituo cha mabasi kilichopo katikati ya jiji na ambacho hakijawahi kupanuliwa kuzidiwa na magari.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha alimwomba Waziri aruhusu kujengwa kwa barabara mchepuko itakayounganisha Uwanja wa Ndege wa Arusha na Barabara ya Dodoma na Ngaramtoni ili kupunguza magari yanayokwenda huko kuingia mjini.

“Magari yanayotoka Namanga yakielekea Babati, Monduli au Ngorongoro yanalazimika kuingia mjini kwanza na yale yanayotoka huko kwenda Namanga pia lazima yaingie mjini. Tungeweza kuyafanya yapitie Barabara ya Dodoma na Namanga bila kulazimika kuingia mjini,” alisema Mkuu wa Mkoa.

Akijibu hilo, Waziri alitoa ruhusa ya kujengwa kwa barabara hiyo na kumtaka Mkuu wa Mkoa kutuma timu ya wathamini kuangalia suala la fidia kabla ya kuanza kazi ya ujenzi.

Wakati huo huo mradi wa upandishaji hadhi wa barabara ya Arusha-Makuyuni, sehemu ya Barabara ya Dodoma na kuwa njia mbili umeanza na tayari nyumba zilizojengwa kando ya barabara ya Ngarenaro, Majengo na Mbauda zimeanza kuvunjwa kupisha ujenzi huo. ■

Magufuli awaonya wafanyakazi wa Mizani kuhusu rushwa

Waziri wa Ujenzi Dkt. John Magufuli ameagiza uchunguzi wa kina ufanywe katika mizani za barabarani, kuhusu matukio kadhaa yanayofanyika yanayoashiria kukithiri kwa rushwa.

“Zaidi ya asilimia 80 ya watendaji wa mizani ni wala rushwa, ndio maana tatizo la uzidishaji wa uzito kwenye magari linaendelea,” alisema. Aliongeza kusema kuwa hata baadhi ya watu wazito wamekuwa wakipiga simu, kuomba watoto wao na ndugu zao wapewe kazi katika mizani jambo linaloashiria kuwepo kwa fedha za haraka haraka. “...na nina hakika wahudumu wengi (wa mizani) wana uhusiano na vigogo, waondoeni. Wafukuzeni,” alisema.

Waziri alitoa maagizo hayo hivi karibuni jijini Arusha alipokuwa akifungua mkutano wa siku tatu uliohusisha wadau wa barabara; Ofisi ya Makamu wa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Kwa mujibu wa Dkt. Magufuli, wakati Serikali inajitahidi kujenga barabara zaidi, zile zilizopo zinaendelea kuharibika kwa haraka kutokana na matumizi mabaya yanayotokana na uzidishaji wa uzito; na faini inayotozwa kwa magari yanayozidisha uzito kuwa ndogo sana. “Faini inayotozwa kwa wanaozidisha uzito haiendani na uharibifu unaofanyika kwenye barabara,” alisema Dkt. Magufuli na kueleza kuwa katika miaka mitatu iliyopita, Mizani imekuwa ikikusanya kiasi cha Sh. bilioni 3 kila mwaka hali inayoonisha kuwa maofisa wa mizani wameweka hicho kama kiwango cha makadirio huku wakiwa wanakula njama na madereva wanaozidisha uzito kwa maslahi yao binafsi.

Dkt. Magufuli aliamuru Wakala wa Barababara Tanzania (TANROADS) kutumia mamlaka yake ya kuajiri na kufukuza kushughulikia tatizo hili. “Ninyi mnayo mamlaka ya kuajiri na kufukuza. Sasa tumieni mamlaka yenu kufukuza zaidi kuliko kuajiri,” alisema na kuongeza kuwa kama jambo hili likifanyika, anaamini asilimia 90 ya maofisa wa mizani ‘watakwenda na maji’.

Fedha za Mfuko wa Barabara

Dkt. Magufuli pia aliwaonya maofisa wanaohamisha fedha zinazotolewa na Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara na kuzitumia kwa matumizi mengine yasiyohusiana na barabara. Alisema tatizo hilo limekuwa kubwa na sasa linahitaji kushughulikiwa, ili kuiwezesha Bodi kutimiza majukumu yake. Alisema kuwa ana taarifa kuwa baadhi ya fedha za matengenezo ya barabara zimekuwa zikitumika kwenye mbio za Mwenge wa Uhuru, kulipia posho za wasimamizi wa mitihani ya Kidato cha Nne au kulipa posho ya mikutano ya Bodi.

“Hii haiukubaliki, natoa wito kwa Bodi kuchunguza na kufanyia kazi suala hili ili kuwachukulia hatua maofisa wote wanaohusika katika matumizi haya yasiyofaa,” alisema Dkt. Magufuli.

Waziri alitaka Bodi kuhakikisha kuwa matokeo ya uchunguzi huo yanapelekwa kwa Wizara husika haraka kwa utekelezaji.

Pia aliwataka makatibu wakuu wa Wizara za Ujenzi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na maofisa wa juu wa TAN-



Mzani wa barabarani eneo la Mikese Morogoro. Waziri Magufuli anasema watendaji wengi wa Mizani ni wala rushwa

ROADS kuwachukulia hatua maofisa waliohusika na kutumia fedha za matengenezo ya barabara kwa matumizi mengine. “Hii ni kinyume cha sheria inayoongoza Mfuko wa Barabara,” alisema, na kuongeza kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma kuna Mkandarasi aliyelipwa mara mbili katika mradi mmoja.

Alisema mifano mingine imetokea katika Halmashauri za Wilaya za Morogoro, Chato, Kishapu, Mtwara, Kigoma, Bihamramulo, Bukoba, Muleba na Misenyi ambapo fedha za Mfuko zilitumika kulipa posho, mafuta ya gari, na matumizi mengine ambayo hayahusiani na matengenezo ya barabara.

“Tatizo hili ni kubwa sana katika nchi hii,” alisema akitoa mfano wa Manispaa za Morogoro na Musoma, Halmashauri za Wilaya ya Mafia, Mwanga, Geita, Chato, Kibondo, Bariadi na Tarime ambako fedha za Mfuko wa Barabara zilitumika kwa mbio za Mwenge na kulipa posho za wasimamizi wa mitihani ya Kidato cha Nne na kununua vifaa ambavyo havihusiani kabisa na ujenzi.

Pia alisema kuwa katika Wilaya ya Chato, fedha za Mfuko zilitumika kuchimba shimo la takataka na kutoa kazi hiyo bila hata kutangaza zabuni. Dkt. Magufuli pia alisema kuwa kuna wakanadarasi wanaofanya kazi chini ya kiwango, hivyo kuchangia katika matumizi mabaya ya rasilimali. “Imetokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ambapo daraja la Kigwe-Ngulugano lilikuwa chini ya kiwango.”

Aliitaka Bodi kuhakikisha kuwa fedha za barabara zinatumika kwa maendeleo ya kijamii na kuichumi ya nchi.

Dar es Salaam: Uwiano ni watu wanne gari kwa moja

Wakazi wa Dar es Salaam wameelezewa kuwa wananunua magari katika kasi ya kutisha ambapo hivi sasa uwiano wa magari

Inaendelea uk. 5

Asemavyo Mhariri

Jarida jipya kwa ajili yako

Mpendwa mdau,

Karibu katika toleo la kwanza kabisa la 'Tanzania Roads', jarida la Bodi ya Mfuko wa Barabara lenye lengo la kukupa habari juu ya kinachoendelea ndani ya Bodi ya Mfuko wa Barabara na sekta ya barabara kwa ujumla.

'Tanzania Roads' ni jarida litakalokuwa likitoka mara mbili kwa mwaka, ikiwa ni kila mwezi wa Novemba na Mei. Jarida litabeba habari mbalimbali kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara na wadau wengine ambao, kwa njia moja au nyingine, wana wajibu mkubwa katika matengenezo ya barabara ambazo ni kichocheo cha kukua uchumi wa Taifa letu.

Mwezi Agosti mwaka jana, kulikuwa na mkutano muhimu kati ya TAMISEMI, Bodi ya Mfuko wa Barabara na wadau wengine uliofanyika jijini Arusha, na kwa kuwa wakati huo tulikuwa katika mchakato wa kuandaa jarida hili, imetokea kwamba tumekuwa na habari nyingi kutoka katika mkutano huo. Ni matumaini yangu kuwa jarida hili litafanya kazi nzuri ya kueleza kilichotokea na pia kuweka kumbukumbu za mkutano huo.

Tafadhali tulettee habari na matukio mbalimbali kutoka katika taasisi yako kwa ajili ya toleo lijalo. Pia tunapokea matangazo ambayo tutayachapisha kwa bei nzuri sana kwako na kwa kuwa jarida hili linawafikia wadau wengi, utakuwa na nafasi nzuri sana ya kuwasiliana nao.

'Tanzania Roads' siyo kama magazeti mengine ya kawaida ambayo unahitaji kuwa na taaluma ya uandishi wa habari ili kuliandikia. Katika Jarida hili hata Mhandisi, Msanifu majengo, ama mtu yeyote mwenye taaluma nyingine anaweza kuandikia. Tulettee habari yako nasi tutaichapisha na kuweza kuboresha zaidi jarida letu siku za usoni.

Natumaini kupata habari na matangazo kutoka kwako katika toleo lijalo.

Christopher Kidanka
Mhariri

Bodi ya Uhariri

Joseph Haule	Mwenyekiti
Kukwe Nyabusalo	Katibu
Chris Kidanka	Mhariri Mkuu
Eliud Nyauhenga	Mhariri Maudhui
Joram Kilemile	Mhariri Msanifu
Ronald Lwakatare	Mjumbe
Matayo Kiwayo	Mjumbe

Ujumbe wa Meneja Mfuko wa Barabara

Kijarida hiki cha 'Tanzania Roads' kitakuwa ni mwanzo wa ukomo wa pengo la mawasiliano lililokuwepo huko nyuma kati ya Bodi ya Mfuko wa Barabara na wadau wake, pamoja na jamii.

Ni kusudi langu kuwakutanisha wale wote ambao kwa namna moja ama nyingine wanahusika kuleta maendeleo ndani ya Bodi ya Mfuko wa Barabara. 'Tanzania Roads' ni njia nyingine zaidi ya mtandao wetu yaani www.roadsfundtz.org) iliyoanzishwa ili kupanua wigo kwa jamii katika kuwasiliana na kujua nini kinaendelea ndani ya Mfuko.

Bodi ya Mfuko wa Barabara ni Taasisi ya umma na tunawajibika kwa jamii na hasa kwa watumiaji wa barabara katika kila tunalolifanya na pia kutoa taarifa ambazo zitasaidia ku fahamisha kazi tunazofanya. Katika toleo hili na mengine yajayo ambayo yatatolewa bure kila baada ya miezi sita; tutatoa taarifa kuhusu utendaji wa Mfuko, masuala yanayohusu Idara ya barabara, maoni ya wadau na habari nyingine zinazofaa kwa wadau wa



Meneja Mfuko wa Barabara,
Joseph Haule

barabara .

Nategemea kuwa watumiaji wa barabara ambao wanahusika kwa karibu na utendaji wa Mfuko, watatumia fursa hii kutoa maoni yao kupitia kijarida hiki.

Nachukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliohusika kwa namna mbalimbali katika kufanikisha maandalizi ya toleo hili jipya la 'Tanzania Roads'.

Ni matumaini yangu kuwa wasomaji wote wa kijarida hiki watafurahia habari zilizo, na watakuwa na kitu cha kuchangia siku zijazo na hivyo kusaidia kuleta faida kwa Nchi na uchumi wake kwa ujumla. Nawakaribisha sana kwa usomaji.

J.O. Haule.

Meneja wa Mfuko wa Barabara.

Salamu za Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara

Mpendwa msomaji,
Ninayo furaha kubwa kuwaletsa salamu kupitia toleo la kwanza la jarida la Bodi ya Mfuko wa Barabara, ambalo, pamoja na mambo mengine litakuwa kiunganishi kati yako na Bodi.

Kwa hakika, kwa wananchi wa kawaida, Bodi ya Mfuko wa Barabara haijulikani sana, kwa kiasi fulani, hali hii ni kutokana na ukweli kuwa Bodi haifanyi kazi zake moja kwa moja na jamii.

Naomba nichukue fursa hii kukujulisha kwa kifupi madhumuni ya kuanzishwa Bodi ya Mfuko wa Barabara, muundo na majukumu yake.

Bunge lilipitisha Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Barabara na Bodi yake kwa Sheria ya Tozo za Barabara ya 1998 (Roads Tolls Act 1998 ammendment No 2) kama ilivyorekebisha na Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta Sura 220 ya mwaka 2006 na kuitwa " Road and Fuel Tolls Act Cap 220. Vilevile Bunge lilipitisha sheria iliyounda Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa sheria ya mwaka 1997 ambayo inalo jukumu la kusimamia matengenezo ya barabara kuu na za mikoa kote nchini.

Kufuatana na sheria iliyounda Mfuko mgawanyo wa fedha zilizokusanya ni kwamba

(i) Kiasi cha asilimia isiyopungua tisini ya fedha iliyowekwa katika Mfuko itatumika kwa utunzaji na matengenezo ya dharura ya barabara zilizoainishwa pamoja na gharama za kiutawala zinazohusiana na shughuli hizo katika Tanzania Bara kulingana na mipango ya utendaji iliyo dhinishwa ambayo imepangwa na: Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa upande wa barabara kuu na mikoa na Mamlaka za Halmashauri kwa upande wa barabara za wilaya na miji.

(ii) Asilimia isiyozidi kumi ya fedha iliyowekwa katika Mfuko itatumika kwa uendelezaji barabara pamoja na gharama za kiutawala katika Tanzania Bara. Matumizi yatafuata mipango na bajeti iliyo dhinishwa na Bunge.

Mgawanyo wa fedha za Mfuko ni kwamba asilimia 7 hugawiwa Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Wakala wa Barabara asilimia 63, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa asilimia 30. Mgawanyo huu hufanywa baada ya gharama za uendeshaji za Bodi kuondolewa.

Majukumu makuu ya Bodi ni kuku-sanya fedha, kuzigawa na kufuatilia ma-

tumizi yake. Bodi ina Wajumbe tisa, kati yao wanne wanatoka Serikalini na Wajumbe watano wanawakilisha sekta binafsi wanatoka katika Asasi za kiraia ambao ni pamoja na Mwenyekiti ambaye huteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka sekta binafsi

Mafanikio

i) Kuongezeka kwa mapato ya Mfuko.

Mapato ya Mfuko ulipoanzishwa mwaka 2000/11 yalikuwa ni T. shs 47.25 bilioni, na yameongezeka hadi kufikia T.shs 406 bilioni mwaka 2011/12 na yanategemewa kuwa T.shs

430 bilioni mwaka 2012/13. Hili ni ongezeko la karibu mara kumi katika kipindi cha miaka 12.

ii) Kuboreshwa kwa ubora wa mtandao wa Barabara.

Hali ya mtandao wa barabara imeimarika zaidi tokea kipindi fedha za matengenezo zimetolewa na Mfuko wa Barabara.

iii) Kuimarishwa kwa ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Mfuko.

Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Mfuko umeimarishwa ili kuhakikisha kunakua na thamani

ya fedha katika kazi za matengenezo ya barabara. Hili limefanyika kwa kuajiri wataalam elekezi

kukagua kazi na kwa Bodi na sekretariati kwenda kukagua jinsi kazi zinavyofanyika. Hili limesaidia kupunguza idadi ya hoja za wakaguzi, ongezeko katika uwezo wa kutumia fedha na ubora wa kazi za matengenezo ya barabara.

Changamoto

Pamoja na mafaniko haya, Mfuko unakabiliana na changamoto zifuatazo;

i) Ukosefu wa fedha za kutosha kufanya matengenezo yote ya barabara zote.

Kuna pengo kati ya mahitaji ya fedha za matengenezo na fedha zilizopo, hivi sasa Mfuko unaweza kugharimia kiasi cha asilimia 70 ya fedha zinazo hitajika kwa matengenezo ya barabara. Hali hii husababisha kuwepo kwa bakaa ya barabara zinazohitaji matengenezo.

ii) Hali ya Mtandao wa barabara sio thabiti.

Barabara nyingi sio za lami ni za changarawe/udongo na sio imara wakati wa mvua au magari yakiongezeka hahari-



*Dr James Wanyancha
Mwenyekiti, Bodi ya
Mfuko wa Barabara*

bika upesi hivyo huhitaji matengenezo ya mara kwa mara.

iii) Kupanda kwa gharama za matengenezo.

Kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi na dizeli pamoja na gharama za vibarua kumesababisha kuongezeka kwa gharama za matengenezo ya barabara. Hali hii ime-sababisha upungufu katika kiasi cha kazi za matengenezo ambazo zingefanywa kwa kiasi kilekile cha fedha ukilinganisha na miaka iliyopita.

iv) Ongezeko katika magari yanayozidisha uzito

Magari yanayozidisha uzito husababisha uharibifu katika barabara na kuzifanya zilazimike kutengenezwa mapema kuliko ambavyo ilipangwa. Fedha zinazotumika kurekebisha hali hii zingeweza kutengeneza maeneo mengine kama hili lisingetokea.

Mipango ya baadaye

Bodi imeandaa mikakati ifuatayo kukabiliana na changamoto hizo;

i) Kutafiti juu ya vyanzo vingine vya mapato ya Mfuko.

ii) Kuwasiliana na Serikali juu ya suala la kuimarisha hali ya mtandao wa Barabara.

iii) Kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi na TANROADS juu ya ufumbuzi wa uzidishaji mizigo.

Nakutakia usomaji mzuri wa jarida letu na hivyo kuendelea kufahamu zaidi kazi zetu za sekta ya barabara kwa ujumla.

Dr James Wanyancha

Mwenyekiti, Bodi ya Mfuko wa Barabara

Changamoto matumizi
fedha za barabara Uk 7

RFB kutumia nyezo
mpya za VfM Uk 8

Wakandarasi
wasimamishwa Uk 6



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TANZANIA ROADS

Toleo Na 001 Machi 2013 - Septemba 2013

JARIDA LA BODI YA MFUKO WA BARABARA

**WAZIRI MAGUFULI
AKEMEA RUSHWA MIZANI**

**RFB yajizatiti
kuboresha huduma**

HALIUZWI